

# HAYA NGOJA NIIMBE

Eric Mwaniki 27/3/2019




**HAYA NGOJA NIIMBE**

Nimeyasikia yale unayotenda, nimeona pia unayotenda kwangu
maisha ni bure bila uwepo wako, hivyo basi kuwa nawe ni vyema,
Moyo wangu una raha, raha tele, kwa yale yote Bwana utendayo

***Haya ngoja niimbe, wimbo mtamu, midundo ya kikwetu vinanda tunakuchezea,***
***niache mimi niimbe, wimbo mtamu, sauti tamu tamu kayamba tunakuchezea.***

Umeniokomboa kwa msalaba wako, ukakufa kwa sababu ya dhambi zangu,
huo ni upendo utokao kwa Baba, we' unanipenda mi' mtumishi wako.
Kwa upendo ninaimba, sifa zako, mi' nihubiri watu wakujue

Ukanitetea ukasimama nami, wewe nuru yangu pia wokovu wangu,
nakutegemea wewe unayeishi, unayetawala vyote vilivyo humu
Mungu wa huruma tele, wastahili, kuheshimiwa pia kutukuzwa

Jina lako litukuzwe lihimidiwe, neno lako litangazwe kwa mataifa,
wakujue wewe na wakupende wewe, wakutumikie ndio ma'na naimba
kwani niimbapo nyimbo, wasikika, unawaguza wageuza nyoyo.